Government of **Western Australia**
Department of **Health**

Mwaka 8 (nane) utaratibu wa chanjo- taarifa ya wazazi

Kwa nini chanjo ni muhimu?

Chanjo huzuia watu kupata magonjwa ya kuambukizwa ambayo hubeba hatari kubwa ya magonjwa, ulemavu na kifo. Chanjo husababisha mwitikio wa kinga ambayo inalinda watu kama wanakutana na ugonjwa tena katika mazingira.

Chanjo zote hivi sasa hupatikana huku Australia ni lazima kupitia vipimo masharti magumu ya usalama kabla ya kupitishwa. Chanjo huendelea kufuatiliwa kwa usalama na ufanisi. Soma sana kuhusu chanjo, usalama na kawaida na madhara machache. healthywa.wa.gov.au/immunisation

Mwaka 8 utaratibu wa chanjo

Katika Australia, mwaka 8 wanafunzi wanapata chanjo za mbure kupitia matandao wa kitaifa ndivyo kuzuia magojwa.

- Mkamba
- Pepopunda
- Kifaduro
- Tetekuwanga
- Virusi vya papiloma

Unaweza kusoma zaidi kuhusu magonjwa hayo na chanjo ambazo hutumika kulinda dhidi yao kwa: healthywa.wa.gov.au/immunisation

Ratiba

Wizara ya Afya ya Australia magharibi (WA) na mitaa la jamii timu ya uuguzi hupeana chanjo kila muhula kwa shule ya mtoto wako kulingana na ratiba ifuatayo:

Ziara ya 1 (kwanza)	Virusi vya papiloma Tetekuwanga
Ziara ya 2 (pili)	Virusi ya papiloma Mkamba
Ziara ya 3 (tatu)	Virusi ya papiloma

Ni nini wazazi wanatakiwa kufanya?

Hii pakiti ya ruhusa ya chanjo imepeanwa kwako kupitia njia ya mtoto wako kwa ratiba ya shule ilioko mwaka 8 (nane) Pakiti ina taarifa na fomu ya ruhusa

Kama mzazi au mlezi unatakiwa ku:

- soma fomu ya ruhusa kwenye pakiti kwa makini na wasiliana na muuguzi wa shule yako kama unahitaji habari zaidi
- jibu sanduku ya rangi nyekundu au kijani kuonyesha ni chanjo gani unakubalia na zile haupeani ruhusa halafu tia sahihi kwenye nafasi iliotolewa.
- toa taarifa kwenye fomu ya ruhusa kuhusu matatizo ya kiafya ambavyo vinaweza kuathiri majibu ya mtoto wako kwa chanjo.
- rudisha fomu kama imekamilika kwa shule **Ata kama unakataa chanjo**.

Muuguzi anaweza kuwasiliana na wewe kama anahitaji taarifa zaidi

Wanafunzi wenye fomu zenye sahihi na zimekamilika peke yake ndio watapewa chanjo.

Siku ya chanjo itatangazwa kwenye barua ya habari ya shule ya kila wiki. Kama mtoto wako hakupata chanjo kwa hio siku utafahamishwa na mbadala utapewa njia zingine za chanjo.

Kabla ya mtoto wako kupewa chanjo

Magonjwa madogo ya kawaida kama homa, joto ya mwili ya chini haipaswi kucheweleshwa chanjo. Hata hivyo katika baadhi za kesi inapendekezwa kwamba chanjo isipeanwe au icheleweshwe kutokana na ugonjwa kadhaa. Mjulishe muuguzi wa chanjo wa shule au shule kama mtoto wako:

- amekuwa na athari kubwa kufuatia chanjo hapo mbeleni.
- Ana historia ya allergy kali ambapo chanjo haifai
- amekuwa na chanjo hai katika mwezi uliopita (kwa mfano kifua kikuu, surua, homa ya manjano)
- amekuwa na sindano ya immunoglobulin au kuongezwa ndamu zima katika miezi mitatu iliyopita
- Ana ugonjwa ambao hupunguza kinga, (kwa mfano leukemia, kansa, HIV / AIDS (ugonjwa wa virusi vya ukimwi) au anapata matibabu yanayoathiri kinga (kwa mfano dawa ya steroid kama vile hydrocortisone au prednisolone, radiotherapy, chemotherapy)
- anaishi na mtu ambaye ana ugonjwa ambao hupunguza kinga au ambaye ana matibabu ambayo hupunguza kinga
- Ni mgonjwa wakati wa chanjo

Huduma baada ya chanjo

Mahali pa sindano inaweza kuwa nyekundu na kuvimba - weka nguo baridi juu yake.

Kuna uwezekano kuwa na maumivu kiasi, homa, kuumwa na kichwa au kuchoka. Kwa maumivu ya kichwa na uchungu, peana paracetamol kama ulivyo aagizwa Maumivu yakizidi muone daktari

Tembelea healthywa.wa.gov.au/immunisation kwa taarifa zaidi kuhusu kawaida na madhara kutokana na chanjo

Shauriana na daktari mara moja kama kuna madhara unayofikiria ni mbaya au isioyotarajiwa

Watoa chanjo zote katika Australia magharibi wanatakiwa na sheria kuripoti athari baada ya chanjo. Wazazi pia wanaweza kupiga ripoti juu ya athari yoyote kubwa baada ya chanjo ama kwa mtandao wa inteneti katika wavvs.health.wa.gov.au, ama kwa kupiga simu kwa kliniki ya chanjo namba Central Immunisation Clinic on 9321 1312

Rekodi za chanjo

Kufuatia chanjo, wanafunzi watapata rekodi za chanjo walizopokea.

Chanjo zote zinazopeanwa kupitia mpango wa shule na rekodi kuwekwa na sehemu ya afya ya shule ya Australia magharibi (WA)

Juu yake, chanjo za HPV zinaandikwa katika daftari ya taifa ya HPV: hpvregister.org.au

Mawasiliano

Klinki ya kati ya chanjo
Numba ya simu 9321 1312 8.30am–4.30pm
Jumatatu mpaka Ijumaa

Daktari wa eneo lako

Eneo lako la afya ya jamii
hospitali au kitengo cha afya ya uuma
healthywa.wa.gov.au/publichealthunits

healthdirect Australia
Namba ya simu 1800 022 222

Taarifa zaidi

Wizara ya Afya
healthywa.wa.gov.au/immunisation

Mpango wa chango Australia
1800 671 811 or immunise.health.gov.au
hpv.health.gov.au/for-parents

Hati hii inaweza kupatikana katika muundo tofauti kutokana na ombi la mtu mwenye ulemavu.

Imetolewa na wizara ya afya ya uuma.
© Wizara ya Afya mwaka wa 2015

Hati miliki kwa mali hii ni jukumu ya Jimbo la Australia Magharibi (WA) isipokuwa imeelezwa vinginevyo. Mbali na haki yoyote kushughulika kwa madhumuni ya, masomo ya kibinafsi, utafiti, kukosolewa kwa utafiti, au mapitio, kama inaruhusiwa chini ya masharti ya *Copyright Act 1968*, hakuna sehemu inaweza kutolewa tena au kutumika kwa madhumuni yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Jimbo la Australia Magharibi (WA).

IMM-013031 OCT'15